**TAPORI**

Ni mtandao wa urafiki duniani kote unaowaleta watoto kwapamoja wanaotoka katika mazingira tofauti tofauti,ambao wanataka watoto wapate nafasi sawa. Wanajifunza kutoka kwa watoto ambao maisha yao ya kila siku ni tofauti na ya kwao. Wanafikiri na kutenda kwa dunia yenye usawa kwa kuanzisha njia ya kuishi ambapo hakuna yeyote atakayeachwa nyuma.

**MAWASILIANO**

12, RUE PASTEUR
95480 PIERRELAYE
FRANCE

**BARUA PEPE**

tapori@tapori.org
taporitanzania@gmail.com

**TOVUTI**

en.tapori.org

# Jarida la tapori

Na. 431, Februari - Aprili 2021

*KILA MMOJA ANAWEZA KUSHIRIKI




## Mpendwa tapori

**Unamjua ndege mvumaji? Ndege huyu mdogo pia anatambulika kwa jina la nyuki-ndege mvumi, ni kwasababu ya umbile lake dogo. Ni mwepesi mno na anaweza kupapata mbawa zake zaidi ya mara mia mbili ndani ya sekunde moja.**

Tulipopokea taaarifa zenu ilitufanya tufikiri zaidi kuhusiana na ndege huyu mdogo. Tulifurahishwa sana kwa mipango yenu ya kuwa na ujirani ambao utakuwa na afya kwa kila mmoja. Kama vile ndege mvumi, mmetuonesha ya kwamba hamuhitaji kuwa wakubwa kuwa na uthubutu na kuwahamasisha watu walio karibu nanyi.



Kuanzia sasa kila mtu anaweza kufanya kidogo!

# Habari kutoka......

## Australia

Kwa mwaka mzima, watoto kutoka shule ya st. Elizabeth iliyopo Brisbane, nchini Australia wamekuwa wanasoma vitabu vidogo vya hadithi. Hapa ni miongoni mwa majibu yao kutokana na hadithi ya Diem, binti mdogo kutoka nchini Vietnam:

Dwapendwa Tapori

Shukurani kwa hadithi yenu nzuri mno inayomhusu Diem, ni hadithi inayokonga moyo. Miongoni mwa marafiki zangu, nimekuwa ni mimi pekee ninayehudhuria shuleni, kwasababu walikuwa wanajifunzia nyumbani. Mafanikio mema! Lucy

## Uingereza


"Ndege alileta ujumbe huu kutoka Cambridge.Nyakati ngumu za kuomba urafiki. Kutakuwa na marafiki-kumbuka wapo hapa kwaajili yako."

## Uispania

Wakati wa Tapori tunakuwa pamoja,watoto kutoka Seville na bibi na babu zao walizungumza kuhusiana na ukosefu wa mimea ya kijani kibichi katika maeno jirani na wao. Alafu kutokana na msaada na msaada kutoka kwa mama zao, watoto waliomba miti kutoka almashauri ya jiji. Walimu wao waliwawezesha vitu vya muhimu vinavyohitajika. Kwa kupitia kila mmoja kushiriki, waliweza kupanda mimea kwa mara ya pili.



## Madagascar



Tangu maadhimisho ya oktoba 17, watoto wamekuwa wakitafuta namna ya kujivunia kwa ujirani wao, kipi wanataka kubadilisha na jinsi ya kufanya ili jitihada zao ziweze kuheshimiwa. Walitaka kila mmoja kushiriki kurudisha mazingira yao kuwa mazuri na mazingira safi ya kijani.

# Kwenye Bodi Tapori wanaeleza

Tangu jarida lililopita, mashua ya Tapori imekuwa inafika kote duniani





## Jamhuri ya demokrasia ya kongo

"Nimeiita mashua yangu jina la utanai la Benjamini Tapori, anaeleza {....} dhumuni la mashua yangu ni kuwatoa wavuvi nje ya bahari ili watupe samaki wa kutosha. Na pia kama kuna kuvunjika kwa meli, kunasaidia kuokoa watu wasizame." **Benjamini, Bukavu**

Haya ni maelezo ya baharia, mashua ya tapori inaenda maeneo tofauti tofauti ambapo watu wanaishi katika lindi la umasikini, kuvuka ziwa kivu kwenda bukavu, kuv uka ziwa Tanganyika kwenda Uvira na pia kuvuka bahari kuu na bahari kwenda kwenye mabara mengine."
**Tapori Kibwe-Goma**



## Burkina Faso


"Mashua yetu inaitwa Zoodo. Zoodo ikiwa na maana ya urafiki zaidi.kupitia mashua ya Zoodo tunaenda kuwafikia watoto wengine ambao wanaishi kando kando ya mto Mouhoun na mto Nazino [....]" **Sakina**


Tutumie mashua yako ili tushiriki katika jarida lijalo.


# TUFANYE UTOFAUTI





## HADITHI YA WATOTO WA BUHOLO (BUKAVU, JAMHURI YA DEMOKRASIA YA KONGO)









Lakini nyumba nyingi katika eneo la Buholo ni ndogo mno kwa watu kuweza kusalia nyumbani. Francine na Nicolas kama watoto wengine kwenye eneo hilo hushiriki kwapamoja kwenye ua /uwanja na majirani zao.Mahala hapo wanakutana na Irbain, Gentil na crispin na kufurahia. Kwapamoja wanamakinika kujenga mifano ya nyumba za vijijini kwa klutumia matope.


ATD
Tunapaswa kusalia nyumbani kwasababu kirusi cha koriona kinauwa watu. Ni vigumu kwetu kupata sabuni,kwahiyo tunatumia majivu kuosha mikono yetu, na hii inatusaidia kubaki safi.
Siku moja, viongozi wa Tapori walitembelea watoto kuona jinsi gani walikuwa wanakabiliana na gonjwa hili la UVIKO-19.




Francine ameguswa sana, anazungumzia tatizo kubwa. Rafiki zake pia wanazungumza. Wote kwa pamoja wanaamua kwenda kuonana na mkuu wa wilaya.




Vielelezo: Maureen Bastian

# shughuli

## wachunguzi

**Inasaidia kufanikisha haki za kijamii na kimazingira!**

Katika Mazingira yako vitu vya muhimu vipo hatarini. Dunia yetu ipo hatarini na kuna fursa sawa kwa kila mmoja. Kama wachunguzi, mnaweza kutambua changamoto hizi na kufanya utofauti.

**Pata beji yako.**

### 1 Angalia karibu yako

Uko wapi :

- Je viumbe hai vyote vinaweza kuishi, kukua na kunawiri (wadudu, wanyama wadogo, maua, miti n.k)? kama sio, kwanini sio?
- Je watoto wote na watu wazima wanapata fursa sawa kwenye (elimu, marafiki, vifaa vya shule, mapumziko n.k)? kama sio, kwanini sio?

### 2 Utafiti wako

Chagua mambo unayotaka kuanza kuyachunguza. Kazi yako ni kwenda kuonana na watu wazazi na kuwafanyia mahojiano. Unaweza ukachagua mtu wa kuandika majawabu ya watu wazima.

### 3 Tambua tatizo

Kupitia kusoma tena majibu mnaweza mkachagua tatizo la msingi kwa pamoja ambalo mnaweza mkalifanyia kazi, liandike kwenye bango.

### 4 Hatua ya kuchukua

Kwa pamoja tuangalie masuluhisho ya tatizo tulilolichagua na kuibuka na suluhu ambayo inaweza kuwa njia ya kutatua tatizo. Pia fikiria kwa umakini kuhusu pengine suluhisho lililochaguliwa ni la kweli, na ni muda gani lingechukua ili kushughulikiwa. Shiriki uzoefu wako pamoja nasi.

Shughuli hii imehamasishwa kwa pamoja na vifaa vya elimu vya oktoba 17 mwaka 2020.

# Karibu tapori

## Jamhuri ya kidemokrasia ya kongo, Goma

Watoto kutoka nyumba ya watoto ya Lutonde walisheherekea siku ya oktoba 17 na watoto wa Tapori na watoto kutoka maktaba ya mtaa. Hatimaye watoto walikuwa na shauku ya kuendelea na kazi zao. Kwa kuendelea na hari hii kundi jipya lilianzishwa. Asanteni sana Lutonde kwa kutuonesha kwamba popote watoto wanapokuwa pamoja wanaweza kufikiria aina ya dunia wanayoipenda, hamasa ya Tapori ipo hapo.



## Peru, Cusco

Kundi la COMIPAZU lilianza mwezi oktoba. Jina lake lilichaguliwa na watoto na lina maana ya "wimbi la urafiki, amani na umoja" kazi yao ya kwanza ilikuwa ni kujaribu mchezo wa penguini (Jarida namba 429) kuhusu haki za kijamii na mazingira.

Ni rafiki wangu wa dhati
Ni nyumba yangu
Ni wa kijani na bluu/buluu
Na yuko hai/anaishi
Ana mapafu na macho madogo
Anatupenda mno
Kwamba ametusamehe
Ndio mana ninataka kukusafisha
unaumwa sana
Kwa hiyo ninashikilia kwako na ninakupenda sayari ya dunia.

**Ana Gabriela**




# Kikundi chini ya darubini: Jamhuri ya Afrika ya kati

## Kugundua maisha ya watoto wa Tapori

Tangu desemba, maisha yamebadilika kuwa juu chini ndani ya Jamhuri ya Afrika ya kati. Ghafla kila kitu kilibadilika. Nchi ikawa wahanga kwa waasi, ambao walitaka kuvuruga uchaguzi. Hali hii ya vita ilikuwa juu ya janga la UVIKO-19: Hakuna shule, amri ya kutokutoka nje, kufungwa kwa masoko n.k.

Kukumbana na hali hii, watoto wamejipanga kuwaunga mkono wazazi wao:

- Watoto katika eneo la Sega huwa wanavuka mto Ubangui asubuhi na mapema kutafuta kuni.
- Watoto wa Tapori kwenye eneo la Walingba waliuza vitu..
- Watoto wa eneo la Kokoro waliulizia kuhusu eneo la ardhi lisilotumika ambalo wangeweza kupanda mboga mboga na viungo..

**Christiano** kutoka Walingba anatushirikisha matarajio yake:
"Natamani vita ingemalizika na amani ingerejea kwenye nchi yangu"



**Jisikie huru kuandika jumbe kwa watoto wa Jamhuri ya Afrika ya Kati!**

# Bustani ya wakati ujao

Kwenye mwaka 2018, Coco Ma Angaya ambaye ni bibi wa msichana mdogo kutoka kwenye kikundi cha tapori kilichopo kwenye visiwa vya Reunion waliokabidhiwa vizazi vya wakati ujao kwa kupewa bustani nzuri ya maua ya Yasmini yaliyochanua. Wakati wa wiki ya kubadilishana maarifa na sanaa, Coco aliwaalika watoto ili wavitunze vitu vyote vinavyowazunguka. Leo vijana wadogo watunza bustani wanaangalia kwa pamoja ni ipi waliita bustani ya wakati ujao.. **Twende tukayagundue.**

**Ukuta wa maonesho ya michoro ya kisanaa ulianzishwa na wakazi wa maeneo jirani.**

"Matumaini yetu kwa mtazamo mpya juu ya watu wanaotoka katika maeneo jirani, kwa ishara tofauti na muunganiko mzuri kati ya watu, mimea na wanyama wadogo kwenye bustani".



Matairi yaliyosindikwa yamekuwa mitungi ya maua.!

**Ronn kozé**, ni duara la mawe, maneno yaliyozunguka kwenye matairi na kwenye mitungi ya maua

## unajua?

Magome ya benzoini hutuliza kikohozi na kutoa hafueni ya kuharisha.







Mmea huu unaitwa ulimi wa mama mkwe.

Chini ya majani kuna mabuu, mijusi,jongoo na viumbe wengine wadogo.

## Jumanne ni siku ya bustani

Kila jumanne makundi huwa na furaha na kufuata moja baada ya lingine kwenda na jembe, kuchimba na kupanda mimea kwenye anga hewa zuri na miongoni mwa wale ambao wameweka aibu mbali kutokana na kusoma pamoja ni miongoni mwa wale wenye shauku kubwa, hata kwa zoezi la umwagiliaji la kila siku wazazi pia huja na kushiriki na kutoa matumaini na ushauri.

**"Tunahitaji mimea inayoweza kuliwa"**, Watoto punde wanasema, punde si punde wamesema hivi, mimea mipya kutoka bustanini kwenda kwenye sahani imepandwa. Katika kipindi cha mavuno, furaha huongezeka kila mmoja huenda na mboga mboga za majani. Mwishoni mwa mwaka maua Yasmini huchanua vizuri sana, na kufanya kila mmoja kujivunia. Katika maeneo jirani zoezi la usafi linaendelea na upandaji unazidi uchafuzi.

## Mavuno

### Mimea tiba au mimea asili ya tiba...

Alovera, mmea wa Rozimeri, shamari tamu, thaimu, mmea wa horseradish, kivumbasi,mnana n.k

### Na bustani ya mboga mboga maharage

Maharage,kabeji,karoti,nyanay, viazi vitamu, hoho, chayote, mihogo, arugula, chainizi n.k

Ndege wa kitropiki ni visiwa vya Reunion, nembo ya ndege unaweza kuitambua kwenye mchoro?